



Sheria za Usalama za Colorado Kwa Watoto Wanaobebwa kwa Gari

Mnamo Juni 2024, Gavana Jared Polis alitia sahihi sheria ambayo inasasisha sheria ya usalama wa watoto ili kuwiana na mapendekezo ya utafiti wa karibuni zaidi kuhusiana na kiti cha gari, kiti cha nyongeza, na matumizi ya ukanda wa kiti kwa watoto. Sheria hizo mpya ambazo zitaanza kutumika Januari 1, 2025 zitawawezesha wanacolorado waende sambamba na mbinu bora zaidi zinazotokezwa za matumizi ya kiti cha gari na kiti cha nyongeza.

Sheria za Colorado za usalama wa Watoto Wanaobebwa Kwa Gari, Kutia ndani Zilizosasishwa Zitakazoanza Kutumika Jan. 1, 2025:

- Colorado, dereva anaweza kuadhibiwa kwa kupewa tiketi ikiwa ana mtoto wa chini ya miaka 18 anayebewba kwenye gari lake bila kiti cha gari, cha nyongeza au ukanda wa kiti.
- Mkanda wowote wa kudhibiti mtoto au ukanda wa kiti ni sharti uwekwe kulingana na maelekezo ya mtengenezaji.
- Watoto ni sharti wafikie urefu, uzito na umri unaohitajika ili kutumia ukanda wa kudhibiti wanaotumia.
- Mikanda yote ya kudhibiti ni sharti ipatane na Viwango vya Jimbo vya Usalama wa Magari. Viti ghushi vya gari vimeenea sana na ni hatari. Ili kuhakikisha ni salama kutumia, tafuta lebo inayoonesha imeidhinishwa kutumika kwa gari.

Viti Vinavyoangalia Nyuma

- Kwa watoto wa chini ya miaka 2, na wenyewe uzito wa **chini ya pauni 40**.
- Ikiwa ipo ni sharti iwe kwenye kiti cha nyuma.
- Kiti cha kuangalia nyuma kinaweza kuendelea kutumika kwa mtoto wa umri zaidi ya miaka 2 na pauni 40 hadi anapopita mipaka ya urefu na uzito wa kiti cha gari(inapendekezwa).

Viti vya Gari Vinavyoangalia Mbele.

- Chini ya Miaka miwili na **zaidi ya pauni 40**.
- Umri wa miaka 2-4 , **na** angalau pauni 20
- Ikiwa ipo ni sharti iwe kwenye kiti cha nyuma.
- Kinachoangalia mbele kinaweza kuendelea kutumika kwa mtoto wa zaidi ya miaka 4 na pauni 40 hadi atakapofikia mipaka ya urefu au uzito wa kiti cha gari (inapendekezwa).

Viti vya Nyongeza

- Umri wa miaka 4-9 **na** angalau pauni 40.
- Ikiwa ipo ni sharti iwe kwenye kiti cha nyuma.
- Unaweza kuendelea kutumia kiti cha nyongeza kwa mtoto mwenye umri wa zaidi ya miaka 9 hadi atakapoweza kutoshea ukanda wa kiti bila kiti hicho.

Ukanda wa Kiti

- Umri wa miaka 9-18.
- Ni sharti atoshee vizuri mkanda wa kiti.

Ukiwa na maswali, tafadhali wasiliana na waratibu wa Car Seats Colorado kwa carseatscolorado@gmail.com.